

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA MAKAMU WA RAIS**



**SHINDANO LA UPIGAJI PICHA ZITOKANAZO NA TAKA ZA PLASTIKI**

Ofisi ya Makamu wa Rais Ofisi ni Kiungo katika utekelezaji wa Mkataba wa Basel wa Umoja wa Mataifa unaohusu udhibiti wa usafirishaji na utupaji wa taka hatarishi baina ya nchi na nchi.

Kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Mkataba wa Basel, Ofisi inawaalika wananchi kushiriki katika Shindano la Upigaji Picha zitokanazo na Taka za Plastiki. Madhumuni ya shindano hili ni kuelimisha na kuongeza uelewa kwa umma juu ya changamoto zitokanazo na taka za plastiki pamoja na taratibu za kukusanya, kuhifadhi, kusafirisha na kuteketeza, kurejeleza taka hatarishi na taratibu zinazotakiwa kisheria.

Shindano hili linahusisha waombaji kutoka nyanja mbalimbali kuanzia watoto, vijana na watu wazima wenye taalamu rasmi na wale wasio na taaluma rasmi katika fani ya upigaji picha.

**Masharti na Vigezo vya Shindano**

1. Picha zinazotakiwa zinaweza kuwa za rangi au nyeusi/nyeupe (black and white), ziwe katika mfumo wa JPEG na ukubwa usiopungua MB 1.5 (pixel 2048x1536 au pixel 1536x2048).
2. Picha hizo ziwasilishwe kwa kutumia fomu maalumu inayopatikana kupitia; [www.basel.int/?tabid=8349](http://www.basel.int/?tabid=8349)
3. Unaweza kushiriki mara tatu
4. Picha inayowasilishwa ni ile iliyopigwa na mshiriki
5. Picha ziwekewe utambulisho ukiwemo jina la aliyemituma, uraia, mawasiliano na anwani ya baruapepe
6. Maombi yazingatie picha halisi iliyopigwa na mshiriki husika kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa

Maombi yote yatumwe moja kwa moja kwa Sekretarieti ya Mkataba wa Basel kabla ya tarehe 30 Septemba, 2020. Washindi wa shindano hili kutoka kila kundi watapatiwa zawadi nono.

Kwa maelezo zaidi kuhusu shindano hili na namna ya kushiriki tafadhali tembelea kiunganishi hiki hapo chini;

<http://www.basel.int/Implementation/Plasticwaste/PlasticWastePartnership.Photocontest/tabid/8348/Default.aspx>

[au](http://www.basel.int/photo-competition)

[www.basel.int/photo-competition](http://www.basel.int/photo-competition)

Kwa maswali au ufafanuzi zaidi kuhusu namna ya kushiriki unaweza kuwasiliana na Bi. Eva Shirima kwa simu namba 0788 181 003.